

FAIDA ZA MATUMIZI YA KINYONGA

- Kufahamu wakati muafaka wa kumwagilia.
- Muda zaidi wa kufanya palizi na shughuli nyingine
- Kutomwagilia mara kwa mara kunachangia upatakinaji zaidi wa maji kwa watumiaji wengine upande wa chini
- Matumizi bora ya mbolea
- Kuongezeka kwa mavuno

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

MKURUGENZI MKUU

TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI

S.L.P. 146

DODOMA

Barua Pepe: info@nirc.go.tz

UMWAGILIAJI NI KILIMO CHA UHAKIKA

**JAMHURI YA MUUNGANO YA
TANZANIA**

TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI



**UHAMASISHAJI WA TEKNOLOJIA YA
KUPIMA UNYEVU KWENYE ARDHI AU
“TEKNOLOJIA YA KINYONGA”**

TECKNOLOJIA YA KUPIMA UNYEVU KWENYE UDONGO(KINYONGA)

Tekinoljia hii hupima uwepo wa unyevu nyevu ndani ya udongo, na kinapima kiasi cha mvutano ambacho mmea unatumia kupata maji kutoka kwenye udongo. Kina taa za rangi nne na hufukiwa ndani ya udongo ili kupima unyevunyevu. (Picha na. 1)



Picha 1. Picha hapo chini inaonyesha ulowekaji wa Kifaa cha kuhisi mvutano wa unyevu na mmea

- Kifaa hiki kitasimikwa pale rangi itakapokuwa imebadilika na kuwa bluu baada ya kulowekwa. Kinyonga kikilowekwa kwenye maji bila kuonyesha rangi ya bluu ujue ni kibovu.
- **Uchimbaji wa Shimo.** Wakati wa kuchimba shimo hakikisha kuwa udongo unaofanana uwekwe pamoja.

Kifaa kinasoma katika kina cha sehemu nne. (Picha na 2).

1. Bluu itakuwa juu
2. Nyeupe/Kijivu itafuatia
3. Nyekundu
4. Nyeusi itakuwa chini kuliko zote



Picha 2. Picha hapo chini inaonyesha kifaa cha kupimia unyevu na rangi zake.

• Usimikaji(1)

Kifaa cha kuhisi unyevunyevu kinasimikwa kwa wima na waya ikibakia juu.

Chimba sentimita 3 zaidi ya kina unachotegemea kupima, mfano kama unataka kupima sentimeta 15 chimba sentimita 18 ilikusudi sentimita 15 ziwe katikati ya kifaa cha kupima unyevunyevu.

• Usimikaji(2)

Kifaa cha kupima unyevunyevu kinaweza chimbiwa kwenye shimo moja kwa kila kimoja au zaidi ya kimoja kuchimbiwa kwenye shimo moja. Picha na. 3). Kuwa mwangalifu wakati wa kufukia kusudi kila kipima unyevunyevu kiwe katikati sehemu kinayotakiwa kupima.



Picha 3. Picha hapo chini ikionyesha usimikaji wa kifaa cha kupimia unyevu ardhini

• Ufukiaji wa shimo (1)

Tumia mti aina ya mwanzi au kifaa chochote ambacho unaona kinafaa kufukia udongo kwa makini ukishindilia vizuri bila kuathiri vifaa vya kupimia unyevunyevu.

Hakikisha umerudishia udongo sehemu yake, udongo wa chini urudi chini na udongo wa juu urudi juu..

• Ufukiaji wa shimo(2)

Wakati wa kufukia shimo hakikisha kwamba shimo limefukiwa usawa wa ardhi kuzuia maji kuingia na kuharibu vipimo. (Picha na. 4)



Picha 4. Picha hapo chini ikionyesha ufukiaji wa shimo lenye kifaa cha kupimia unyevu

• Usomaji (1)

Unganisha waya zote kwa kufuata rangi kama ifuatavyo:-

- Bluu kwa Bluu
- Nyeupe kwa nyeupe
- Nyekundu kwa nyekundu
- Nyeusi kwa nyeusi

• Usomaji (2)

- Hakikisha sola paneli imeelekezwa kwenye mwelekeo wa jua, funika sola paneli na mkono kwa muda wa dakika tano ukitoa mkono kinyonga inaanza kusoma kwa kuonesha rangi na kama mwanga ni kidogo huenda ikashindwa kusoma mpaka mwanga utakapokuwa wa kutosha.

- Hakisha umechimbia sehemu salama.

Kinyonga kichimbiwe sehemu ambayo ni sala- ma isiyosumbuliwa na ambayo haikanyagwi mara kwa mara wakati wa kuhudumia shamba